www.tea.or.tz

# MFUKO WA ELIMU

Toleo la 3
Aprili - Juni
2024

## TEA NA EATV KUSHIRIKIANA KAMPENI YA NAMTHAMINI




>> TEA YAPATA MWENYEKITI MPYA WA BODI

>> WADAU WA ELIMU MKOANI TANGA WAIPONGEZA TEA

*"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu Ya Elimu"*

# KUHUSU TEA

**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)** ni Taasisi ya umma iliyoanzishwa kwa Sheria ya Bunge ya Mfuko wa Elimu Na. 8 ya 2001 chini ya kifungu cha 5 (1) ili kuratibu na kusimamia Mfuko wa Elimu, ulioanzishwa kwa sheria hiyo hiyo. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho mwaka 2013.

Madhumuni ya Mfuko wa Elimu ni kuongeza nguvu za Serikali katika kugharimia miradi ya elimu ili kuinua ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa, katika ngazi zote za Elimu kwa Tanzania Bara na Elimu ya Juu kwa Tanzania Zanzibar.

### Mfuko wa Elimu

Mfuko wa Elimu unapokea rasilimali fedha na vifaa ambazo hukusanywa na kuratibiwa na Mamlaka ya Elimu Tazania (TEA) kwa lengo la kufadhili miradi ya elimu nchini kutoka vyanzo mbalimbali ndani na nje ya nchi.

TEA imepewa jukumu la kuhamasisha wadau mbalimbali nchini na nchi za nje kuchangia rasiimali mbali mbali kwa lengo la kusaidia juhudi za Serikali kuinua ubora, na kuongeza upatikanaji wa elimu kwa usawa



## DIRA

Washiriki wa kampeni hii watapata faida zote zinazopatikana kwa wachangiaji wa sekta ya elimu kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa ikiwa ni pamoja na kutambuliwa na kuorodheshwa katika Rejista ya Kudumu ya wachangiaji wa Mfuko wa Elimu.



## DHAMIRA

Kutafuta rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya Mfuko wa Elimu na kuzigawa rasilimali hizo kwa ufanisi katika kufadhili miradi ya elimu ili kuboresha upatikanaji wa elimu bora na ujuzi kwa usawa.

# YALIYOMO


Salaam za Mkurugenzi Mkuu.................................................01

TEA na EATV kushirikiana kampeni ya NAMTHAMINI.........02

TEA yapata mwenyekiti Mpya wa Bodi.................................03

Wadau wa elimu mkoani Tanga waipongeza TEA...............04

Habari katika picha: kikao cha tatu (3) cha baraza la wafanyakazi wa TEA............................................................05

Serengeti yaishukuru TEA kwa miradi ya elimu.....................07

TEA kushiriki urejeshaji wa miundombinu ya elimu wilayani Rufiji..........................................................................08

Solla Mtumishi Hodari wa TEA 2024....................................09

Toka chumba kimoja hadi kiwanda cha kuzalisha mvinyo..................................................................10


# TIMU YA UHARIRI

**Mwenyekiti:** Masozi Nyirenda

**Mhariri:** Bestina Magutu

**Wachangiaji:** Eliafile Solla

Joyce Minja

# ANUANI:


**Mamlaka ya Elmu Tanzania(TEA)**

**S. L.P 2516, Dodoma- Tanzania**

**Barua pepe: info@tea.or.tz,**

**Tovuti www.tea.or.tz,**

**Instagram: Officialteatz,**




## SALAAM ZA MKURUGENZI MKUU

**Karibu katika Toleo la Tatu la Jarida la Mfuko wa Elimu!**

Toleo hili linaangazia juhudi zilizotekelezwa katika robo ya nne ya Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, kuanzia Aprili hadi Juni 2024. Moja ya mafanikio makubwa katika kipindi hiki ni kusainiwa kwa makubaliano ya ushirikiano baina ya Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na kituo cha utangazaji cha East Africa Television (EATV) katika kuendesha kwa pamoja kampeni ya Namthamini. Kampeni hii imelenga kuimarisha na kuweka mazingira rafiki kwa wanafunzi wa kike.

Kupitia kampeni hii, TEA na EATV wanahamasisha uchangiaji wa rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya vyoo na upatikanaji wa maji safi na salama. Lengo ni kuhakikisha wanafunzi wa kike wanapata mazingira safi, hasa wakati wa hedhi. Hivyo inalenga kuwapatia wanafunzi taulo za kike, matundu ya vyoo na maji safi na salama.

TEA inatilia mkazo kampeni hii kwani inatoa fursa kwa wadau wa elimu kote nchini kushiriki kikamilifu katika kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi wa kike hatua ambayo italeta matokeo chanya kwa wanafunzi hao na kwa taifa letu kwa ujumla.

Washiriki wa kampeni hii watapata faida zote zinazopatikana kwa wachangiaji wa sekta ya elimu kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa ikiwa ni pamoja na kutambuliwa na kuorodheshwa katika Rejista ya Kudumu ya wachangiaji wa Mfuko wa Elimu.

Aidha, wachangiaji watapewa Hati ya Utambuzi wa Uchangiaji wa Elimu (Certificate of Educational Appreciation - CEA) ambayo inaweza kutumika kuombea nafuu ya kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kwa mujibu wa Kifungu cha **16 (1)** cha Sheria ya Kodi ya Mapato **Sura 332,** marejeo ya mwaka **2019**.

Tunawahimiza wadau wote wa sekta ya elimu kushiriki katika kampeni hii yenye manufaa makubwa, ambayo inaendeshwa kwa ushirikiano na Mfuko wa Elimu wa Taifa na EATV.

**Dkt. Erasmus F. Kipesha**
*Mkurugenzi Mkuu-TEA*

# TEA NA EATV KUSHIRIKIANA KAMPENI YA NAMTHAMINI



*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Dkt. Erasmus F. Kipesha (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa EATV Regina Mengi wakisaini makubaliano ya Ushirikiano (MoU) kwa ajili ya utekelezaji wa pamoja wa kampeni ya NAMTHAMINI.*

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na kituo cha utangazaji cha EATV wanashirikiana katika uendeshaji wa kampeni maalum ya Namthamnini inayolenga kuweka mazingira rafiki ya kujifunza kwa wanafunzi wa kike.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya Mkurugenzi Mkuu wa TEA, Dkt. Erasmus Kipesha na Mkurugenzi Mtendaji wa EATV Bi. Regina Mengi kusaini Makubaliano ya Ushirikiano (MoU) katika hafla fupi iliyofanyika Makao Makuu ya EATV Mikocheni, Dar es Salaam tarehe 16 Juni, 2024.

Kupitia kampeni hii, TEA inashirikiana na EATV kuhamasisha uchangiaji wa rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo na upatikanaji wa maji safi na salama ili kuwawezesha wanafunzi wa kike kuwa na hedhi salama.

Akizungumza kwenye hafla hiyo Dkt. Kipesha alisema, Mamlaka imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali kutafuta rasilimali fedha na vifaa kwa ajili ya kufadhili miradi ya elimu kwa lengo la kusaidia jitihada za Serikali za kuboresha mazingira ya kujifunza na kufundishia.

Alitaja faida za wadau kuchangia kupitia Mfuko wa Elimu wa Taifa kuwa ni pamoja na kupata Hati ya Utambuzi wa Uchangiaji wa Elimu (Certificate of Educational Appreciation- CEA) kwa mujibu wa Kifungu cha 12 cha Sheria ya Mfuko wa Elimu ya mwaka 2001.

Mdau ataweza kutumia hati ya CEA kuombea nafuu ya kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mujibu wa Kifungu cha 16 (1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato Sura 332 na marejeo ya mwaka 2019.

Faida nyingine ni mdau kutangazwa na kutambuliwa kitaifa, ambapo mchangiaji huandikwa katika rejesta ya kudumu ya wachangiaji wa elimu.

Namthamini ni kampeni iliyoanzishwa na kituo cha utangazaji cha East Africa TV/Radio Limited mwaka 2017 kwa ajili ya kuchangisha taulo za kike kwa wanafunzi wenye uhitaji mashuleni.

Kampeni hii ilikuja baada ya tafiti kuonyesha wanafunzi wengi wa kike wanashindwa kununua taulo za kike katika siku zao za hedhi hali inayoathiri mahudhurio ya masomo kwa wastani wa siku 3 mpaka 7 kwa mwezi.

# TEA YAPATA MWENYEKITI MPYA WA BODI



*Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Elimu Tanzania,* ***Dkt. Leonard Akwilapo***

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) impata Mwenyekiti mpya wa Bodi baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kumteua Dkt.Leonard Douglas Akwilapo kushika wadhifa huo kuanzia tarehe 15 Juni 2023.

Dkt. Akwilapo anachukuwa wadhifa huo baada ya aliyekuwa Mwenyekiti wa Bodi ya TEA, Prof. Maurice Mbago kumaliza muda wake. Dkt. Akwilapo ni Katibu Mkuu Mstaafu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kwa sasa ni Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dodoma.

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ni Taasisi ya umma inayofanya kazi chini ya usimamizi wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

TEA inaratibu Mfuko wa Elimu wa Taifa ambao jukumu lake kuu ni kutafufa rasilimali fedha na vifaa, kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo ya sekta ya Elimu ndani na nje ya Tanzania ili kusaidia jitihada za Serikali za kuboresha miundombinu ya elimu kwa lengo la kuongeza ubora wa elimu na upatikanaji wake kwa usawa.

# WADAU WA ELIMU MKOANI TANGA WAIPONGEZA TEA

Mkuu wa Mkoa wa Tanga Balozi. Dkt. Batilda Salha Burian ameipongeza Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kwa mchango wake muhimu katika uboreshaji miundombinu ya Elimu Mkoani humo.

Dkt. Burian alitoa pongezi hizo alipotembelea banda la TEA katika maonyesho ya wiki ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika katika viwanja vya Shule ya Sekondari Popatlal Jijini Tanga kuanzia tarehe 25 hadi 21 Mei 2024.

Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 miradi mitano yenye thamani ya **Sh. Milioni 473,369,976** inatekelezwa kupitia ufadhili wa Mfuko wa Elimu wa Taifa  Mkoani humo. Miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa madarasa tisa katika Shule za Msingi za Kwamkole, Madanga na Mlambambani kwa thamani ya **Sh. Milioni 220,117,920** ambapo kila shule  imenufaika na madarasa matatu yanayojengwa kwa **Sh.  Milioni 73, 372, 640.**

Aidha, shule ya Sekondari Mtindiri ilinufaika na ujenzi wa matundu 24 ya vyoo kwa gharama ya **Sh. Milioni 51,334,056** wakati Shule ya Msingi ya Moa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga ilinufaika na ujenzi wa nyumba nne za walimu zenye thamani ya **Sh. Milioni 201, 918, 000**

Aidha, Afisa Elimu Taaluma Korogwe Mji Bi. Anna Gambela alisema Halmashauri ya Korogwe Mji imenufaika na ufadhili wa ujenzi wa maabara ya sayansi katika Shule ya Sekondari ya Semkiwa.

"Kabla ya msaada huo wa maabara tatu kwenye shule hiyo ambayo ni mpya ikiwa na wanafunzi zaidi ya 160 wa kidato cha kwanza na cha pili haikuwa na maabara lakini ufadhili wa TEA umewezesha kuanza na kuongezeka mafunzo kwa vitendo". Ameongeza Bi. Gambela wakati alipotembelea banda la TEA.

Maonyesho hayo ambayo yaliandaliwa chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yalihusisha taasisi  mbali mbali za masuala ya elimu na mafunzo  yaliongozwa na kauli  mbiu ya ***Elimu, Ujuzi na Ubunifu kwa Uchumi Shindani***




*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) Dkt. Erasmus F. Kipesha akitoa maelezo kuhusu majukumu ya TEA kwa Mkuu wa Mkoa wa Tanga Balozi Dkt. Batilda Burian alipotembelea banda la mamlaka katika maadhimisho ya wiki ya Elimu, Ujuzi na Ubunifu yaliyofanyika katika viwanja vya shule ya sekondari Popatlal Jijini Tanga.*

# HABARI KATIKA PICHA: KIKAO CHA TATU (3) CHA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA TEA

Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) tarehe 24 Juni 2024 walikutana katika kikao cha tatu cha baraza la pili la wafanyakazi kilichofanyika mjini Morogoro chini ya Mwenyekiti wake Dkt. Erasmus Kipesha ambaye pia ni Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo.

Katika kikao hicho wajumbe walipitia na kujadili utendaji wa TEA katika Mwaka wa Fedha wa 2023/2024. Katika kikao hicho Bi. Mwanaisha Komba alichaguliwa kuwa Katibu wa Baraza la Wafanyakazi wa TEA na Lusungu Kaduma kuwa Katibu Msaidizi. Uchaguzi huo umefanyika baada ya aliyekuwa Katibu wa Baraza hilo Bw. Aidan Lucas kupata uhamisho kutoka TEA kwenda taasisi nyingine.




*Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi Dkt. Erasmus F. Kipesha akiongoza kikao cha tatu cha Baraza la pili la watumishi wa TEA kilichofanyika katika ukumbi wa TAIFORI Mjini Morogoro*



*Wajumbe wa Baraza la Watumishi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) wakishiriki kikao cha tatu cha Baraza la pili kilichofanyika katika ukumbi wa TAIFORI Mjini Morogoro.*

# HABARI KATIKA PICHA: KIKAO CHA TATU (3) CHA BARAZA LA WAFANYAKAZI WA TEA




*Bw. Lusungu Kaduma akizungumza baada ya kuchaguliwa kuwa Katibu Msaidizi wa Baraza la Wafanyakazi la Mamlaka ya Elimu Tanzania katika kikao cha cha tatu cha Baraza la pili kilichofanyika katika ukumbi wa TAIFORI Mjini Morogoro*



*Bi. Mwanaisha Komba akizungumza bada ya kuchaguliwa kuwa Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la Mamlaka ya Elimu Tanzania katika kikao cha cha tatu cha Baraza la pili kilichofanyika katika ukumbi wa TAIFORI Mjini Morogoro.*

# SERENGETI YAISHUKURU TEA KWA MIRADI YA ELIMU



*Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA - TEA Bw. Emmanuel Shirima (kulia) akipokea cheti cha shukrani kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa TEA kutoka kwa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, Mhe. Musa Magasi Mseti aliyekikabidhi kwa niaba ya Halmashauri.*

Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti Mkoani Mara imetunuku cheti cha shukrani kwa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) kutokana na kufadhili miradi ya kuboresha miundombinu ya elimu katika Halmashauri hiyo.

Cheti hicho cha shukrani kimekabidhiwa katika ofisi za TEA Jijini Dodoma tarehe 3 Juni 2024 ambapo Diwani wa Kata ya Morotonga, Mhe. Musa Magasi Mseti alikikabidhi kwa niaba ya Halmashauri.

**"TEA imekuwa mdau mkubwa wa kufadhili miradi ya kuboresha miundombinu ya elimu katika Halmashauri ya Serengeti na katika kata yangu Shule na Sekondari ya Morotonga imepata ufadhili wa ujenzi wa matundu 24 ya vyoo hivyo kupunguza uhaba wa matundu ya vyoo".** Aliongeza.

Miradi mingine iliyofadhiliwa na TEA katika Mkoa wa Mara ni pamoja na ujenzi wa nyumba nne za walimu katika Shule ya Msingi Kitembere kwa thamani ya **Sh. Milioni 201,918,000**, ujenzi wa Bweni katika Shule ya Sekondari Kianyari lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 80 kwa thamani ya **Sh. Milioni 141, 934,320** na ujenzi wa maabara mbili za Sayansi katika shule ya Sekondari Mapinduzi zenye thamani ya **Sh. Milioni 218,117,044.**

Akipokea cheti hicho cha shukrani kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu, Mkuu wa kitengo cha TEHAMA na Takwimu wa TEA, Bw. Emmanuel Shirima amekumbusha wanufaika wanaopata ufadhili wa miradi kuhakikisha inatekelezwa kwa ufanisi wa hai ya juu.

# TEA KUSHIRIKI UREJESHAJI WA MIUNDOMBINU YA ELIMU WILAYANI RUFIJI

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda amesema Serikali itahakikisha miundombinu ya elimu iliyoharibiwa na mafuriko Wilayani Rufiji Mkoani Pwani inarejeshwa kwa haraka kuwezesha wanafunzi kuendelea na masomo.

Akizungumza na waathirika wa mafuriko katika kijiji cha Muhoro na Chumbi B Wilayani Rufiji Mkoani Pwani amewahimiza wazazi kupeleka wanafunzi katika shule zilizo karibu na maeneo waliyopo ambazo hazijaathiriwa na mafuriko wakati taratibu za kurejesha miundombinu ya shule zilizoathiriwa na mafuriko zikifanyika.



*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda (wa pili kulia) akiongea na wananchi na viongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kufuatia maafa yaliyosababishwa na mafuriko wilayani humo ili kuhakikisha wanafunzi wote walioathirika wanapata msaada wa haraka na kuendelea na masomo.*



*Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda (katikati) akisikiliza taarifa ya maafa yaliyosababishwa na mafuriko Wilayani Rufiji kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani Mhe. Abubakari Kunenge (kushoto). Kulia ni Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sanyansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo.*

"Mwanafunzi yeyote anayepelekwa kwenye shule jirani ya zile zilizoathirika apokelewe na aendelee na masomo huku taratibu nyingine zikifuata ikiwemo uhamisho", amesema Prof. Mkenda

Amesema miundombinu ya elimu itajengwa upya ikiwemo madarasa, mabweni, vyoo, nyumba za walimu na shule mpya ya sekondari ya ufundi ambayo ni miongoni mwa shule 26 za mafunzo ya amali ambazo Serikali inaanza kujenga hivi karibuni kwa ajili ya kutekeleza Mtaala mpya.

Katika ziara hiyo Prof. Mkenda aliambatana na Kaimu Mkurugenzi Huduma za Taasisi wa Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) CPA. Mwanahamis Chambega ambaye alipewa maelekezo ya TEA kuchukua hatua za haraka na kushiriki katika zoezi la urejeshaji wa miun-



*Kaimu Mkurugenzi wa Huduma za Taasisi Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) CPA. Mwanahamis Chambega akisaidiwa kushuka kwenye boti alipotembelea baadhi ya shule zilizoathirika na mafuruko Wilayani Rufiji Mkoani Pwani.*

# SOLLA MTUMISHI HODARI WA TEA 2024



***Eliafile Lucus Solla***
*Afisa Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma*

Tarehe Mosi mwezi Mei kila mwaka huadhimishwa kama Siku ya Wafanyakazi Duniani. Siku hii husherehekewa kwa njia tofauti kulingana na mazingira na sehemu husika.

Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazoadhimisha siku hiyo ambapo hutambua mchango na nafasi ya watumishi katika kuleta maendeleo ya nchi. Kama sehemu ya maadhimisho taasisi za umma na zile za binafsi hutumia siku hiyo kutambua jitihada za watumishi wao ambapo pamoja na mambo mengine hutoa tuzo kwa Watumishi Hodari.

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) pia iliendesha zoezi la kumtambua Mtumishi Hodari kwa mwaka 2024 kwa kufuata taratibu, kanuni na miongozo iliyowekwa ambapo Bi. Eliafile Solla Afisa Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma alichaguliwa.

Akizungumza kwa furaha baada ya kuchaguliwa Bi. Solla ameshukuru Menejimenti ya TEA na watumishi wenzake na kuahidi kuendelea kuwa mwadilifu na mchapa kazi.

Meneja Rasilimaliwatu na Utawala Bi. Alice Lukindo ambaye ofisi yake inaratibu zoezi la kumpata mfanyakazi hodari amempongeza Bi. Solla ambapo amesema kwa mujibu wa taratibu mtumishi hodari wa mwaka hupewa cheti na fedha.

# TOKA CHUMBA KIMOJA HADI KIWANDA CHA KUZALISHA MVINYO



*Lisa Mkuyu Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni ya Roselyne akiwa katika eneo la kiwanda Nzuguni Jijini Dodoma.*

Lisa Mkuyu (24) na Witness Jacob (30) wamejikita katika ujasiriamali wa kutengeneza mvinyo wa zabibu kwa miaka mitano sasa wakiendesha shughuli zao katika jiji la Dodoma.

Wahitimu hao wa masomo ya diploma katika masuala ya uongozi kutoka chuo cha Masomo ya Biashara cha CBE Dodoma kwa pamoja wanaendesha kampuni hiyo ya kuzalisha mvinyo inayofahamika kama Roslyne katika eneo la viwanda lililoko kata ya Kizota Jijini Dodoma.

Bi. Lisa ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni hiyo amesema alivutiwa na masuala ya usindikaji tangu akiwa binti mdogo kwa vile bibi yake alikuwa msindikaji pia.

Safari yao ya uzalishaji ilianza mwaka 2019 wakiwa bado wanafunzi katika chuo. "Wakati tunaanza mwaka 2019 tulifanyia uzalishaji nyumbani ambako tulikuwa na chumba kimoja cha kufanyia kazi hiyo lakini kuanzia mwezi Agosti 2023 Serikali kupitia Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo Nchini (SIDO) limetupatia eneo la uzalishaji ambalo limetengwa kwa ajili ya viwanda huko Kizota Jijini Dodoma "anasema Lisa.

Wajasiriamli hao vijana wanakiri kuwa mafunzo ya kuendeleza ujuzi chini ya Mfuko wa Kuendeleza Ujuzi (SDF) uliokuwa ukiratibiwa na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) umechangia sana kukuza biashara yao kwani walikuwa miongoni mwa wanufaika 400 waliopata mafunzo ya kuendeleza ujuzi kupitia SIDO Dodoma. Kupitia mafunzo hayo yaliyoendeshwa mwaka 2000 Lisa na Witness walipata ujuzi na stadi za usindikaji wa mazao mbali mbali ikiwa ni pamoja na usindikaji wa zao la zabibu.

Lisa anasisitiza kuwa baada ya kupata mafunzo hayo walithubutu kuanzisha kampuni ambayo imeendelea kukua ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani elfu moja mwaka 2020 hadi kufikia tani elfu tatu kwa mwezi mwaka 2024.

"Wakati tunaanza tulikuwa tunatumia vinu vya mkono kutwanga zabibu ili kupata mchuzi wa zabibu tuliotumia kutengeneza mvinyo lakini kwasasa tumenunua mashine ya kukamua kutoka nchini Italia mwaka 2022.

Mkurugenzi huyo mtendaji wa Kampuni ya Roslyne amesema mipango yao ya baadaye ni kujenga kiwanda chao ambapo kwa sasa wamepanga katika eneo la viwanda la Serikali Jijini Dodoma.

Wanufaika hao wa SDF walipata fursa ya eneo la kiwanda katika eneo la viwanda la Serikali linalosimamiwa na SIDO Dodoma baada ya kuingia katika kinyang'anyiro cha kupewa eneo hilo na wajasiriamali wengine watano ambapo waliibuka washindi na kukabidhiwa eneo hilo la kuzalishia mvinyo.

Katika miezi minne ya mwanzo Serikali iliwapa eneo hilo pasipo malipo ikiwa ni sehemu ya kuwasaidia kujiimarisha na baada ya miezi hiyo walianza kulipa ada ya pango Sh. 300,000 kila mwezi.

Witness Jacob ambaye ni Meneja Mauzo na mmiliki mwenza wa kampuni hiyo anasema idadi ya watumishi walioajiriwa katika kampuni ya Rosylne imeongezeka kutoka watumishi wanne (4) mwaka 2022 hadi watumishi 17 kwa sasa hatua ambayo wamesema inachangiwa na kukua kwa soko la bidhaa zao

Wamiliki hao wamedhamiria kufikia soko la kimataifa hasa kwa kuwa sasa wako katika hatua za mwisho za kupata cheti cha ubora cha Shirika la Viwango Tanzania (TBS).

**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)**
**S.L.P. 2516, Dodoma Tanzania.**

info@tea.or.tz www.tea.or.tz officialteatz


*"Changia Mfuko wa Elimu, Boresha Miundombinu Ya Elimu"*